# TAASISI YA MAFUNZO YA AFYA AMENYE - MBEYA

**Namba za Simu** +255742164518 / +255766963739 **Barua Pepe:** amenyetraining@gmail.com
**Anuani**: S.L.P 26 Mbeya, **Eneo:** Mbeya Mjini, Airport ya Zamani **Tovuti:** www.amenyeinstitute.ac.tz


**Jina la Mwanafunzi**

**...............................................................**

**Anuani ya Mwanafunzi.**

**……………………………**

**………………………**

**YAH: UTHIBITISHO WA KUJIUNGA NA CHUO KWA MWAKA WA 2026/2027.**

Chuo cha ya Afya Amenye, Ni taasisi iliyosajiliwa na kupewa ithibati na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi **(NACTVET)** na kuthibitishwa na Wizara, na Mabaraza mengine ya kitaaluma kwa usajili namba **REG/HAS/134.** Ili kutoa mafunzo katika kozi mbalimbali za Afya.

Mkuu wa chuo anapenda kukupongeza kwa kuchaguliwa kujiunga na chuo kwa mwaka wa masomo 2026/2027, kwa kozi ya **Medical Laboratory Sciences (**Maabara Tiba).

Muda wa masomo ni **miaka mitatu (3)**. **Muhula wa kwanza utaanza tarehe 31/08/2026.** Hivyo, unatakiwa **kuripoti chuoni kuanzia tarehe 24/08/2026** Kwa ajili ya usajili na mafunzo ya utangulizi. Mafunzo ya utangulizi (Orientation) yataanza rasmi tarehe **25/08/2026**.

Kipindi cha kuripoti chuo, Ofisi ya Udahili na usajili watahakiki nyaraka zote zinazohitajika. Tafadhali zingatia kuwa ni kosa kisheria kutoa taarifa za uongo kwa ajili ya udahili na kufanya hivyo kutapelekea kufutwa moja kwa moja kwa udahili wako na kuchukuliwa hatua za kisheria.

Aidha, Nipende kukupongeza kwa kupata nafasi hii na kukutakia mafanikio mema pamoja na maisha mazuri ya chuo katika masomo yako. Umechaguliwa kusoma katika chuo bora kwa mafunzo ya afya nchini Tanzania, hivyo unatarajiwa kujitoa kikamilifu katika masomo yako ili kutimiza ndoto zako.

Imetolewa na

AMENYE HEALTH TRAINING INSTITUTE P.O.Box 26 MBEYA

Ayoub Ezekiel Tuya

**Mkuu wa Chuo.**

**Viambatisho Vingine katika barua hii ni:**

- *Maelekezo ya Kujiunga na Chuo (Joining Instructions).*
- *Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form).*
- *Fomu ya Uthibitisho wa Mzazi/Mlezi au Mfadhili wa Mwanafunzi.*

## FOMU YA MAELEKEZO.

### SIFA ZA KUJIUNGA.

Muhitimu wa kidato cha nne mwenye ufaulu wa angalau alama **"D"** au zaidi kwa **masomo manne (4)** yasiyo ya dini, yakiwemo **Kemia, Baiolojia, Fizikia au Engineering Science au Hesabu na Kiingereza.**

### MAHALI CHUO KILIPO.

**Chuo kipo Mbeya Mjini, Airport ya Zamani,** Kwa usafiri wa daladala unaweza kushukia Kabwe au Mwanjelwa, Na kupanda bajaji zinazokuja Airport ya zamani au Chuo cha Afya Amenye. Na kama unatoka mkoani au wilaya za nje ya Mbeya mjini, ukishuka stendi kuu au stendi ya nanenane panda daladala na ushukie kabwe au Mwanjelwa, na upande bajaji zinazokuja Airport ya zamani na ulizia chuo cha Afya Amenye.

### MAHITAJI YA USAJILI.

Wakati wa usajili Mwanafunzi Unapaswa kuja na mahitaji yafuatayo

- **i.** Nakala mbili (2) za cheti cha Kidato cha Nne (CSEE).
- **ii.** Picha mbili (2) za pasipoti za rangi (passport size) za hivi karibuni, zikiwa na jina lako nyuma.
- **iii.** Nakala mbili (2) za cheti cha kuzaliwa au hati ya kiapo (affidavit).
- **iv.** Fomu ya Uchunguzi wa Afya iliyojazwa kikamilifu (ambayo imeambatanishwa kwenye fomu hii).
- **v.** Stakabadhi (Risiti) zote halali za malipo (Bank pay-in Slips).

### MAHITAJI MENGINE:

- **vi.** Ndoo ya kudekia na Mfagio.
- **vii.** Rimu mbili (2), zote mbili wakati unaripoti.
- **viii.** Boksi mbili (2) za glovu, zote mbili wakati unaripoti.

**ZINGATIA:** Kitambulisho cha Mwanafunzi kitatolewa baada ya kukamilika kwa taratibu zote za usajili.

**MALIPO YA ADA NA MICHANGO MINGINE.**

Ada zote zinapaswa kulipwa kwenye akaunti rasmi za taasisi kama zilivyoainishwa. Mwanafunzi anatakiwa kuja na stakabadhi halali za benki wakati wa usajili.

**Malipo yote yanayofanyika kwenye akaunti za taasisi hayatarudishwa (No refund).**

**MUUNDO WA MALIPO YA ADA KWA WANAFUNZI WA MWAKA WA KWANZA KWA KOZI YA MAABARA TIBA (MEDICAL LABORATORY SCIENCES) MWAKA 2026/2027.**

| **MAELEZO** | **KIASI** | **AKAUNTI NAMBA YA MALIPO** |
|---|---|---|
| ADA YA MASOMO | 1,400,000/- | **Namba ya Akaunti:**<br>0150388644200 – CRDB<br>**Jina la Akaunti:**<br>Amenye Health Training Institute |
| **MICHANGO MINGINE** | **KIASI** | **AKAUNTI NAMBA YA MALIPO** |
| Practical | 340,000/= | Hulipwa kupitia akaunti hii:<br>**Jina la Akaunti:**<br>Amenye Health Laboratory<br>**Namba ya Akaunti :**<br>0150422045300 – CRDB |
| Stationary | 50,000/= | |
| Kitambulisho | 10,000/= | |
| Usajili | 20,000/= | |
| Library | 50,000/= | |
| Tahadhali | 50,000/= | |
| Serikali ya Wanafunzi | 10,000/= | |
| Rotation | 250,000/= | |
| Mtihani wa Ndani | 185,000/= | |
| **Jumla Ndogo** | **965,000/** | |
| **JUMLA KUU** | **2,365,000/-** | |
| **MITIHANI YA WIZARA NA UHAKIKI UBORA** | | Hulipwa kupitia akaunti hii:<br>**Jina la Akaunti:**<br>Amenye Health Laboratory<br>**Namba ya Akaunti :**<br>0150422045300 – CRDB |
| Mtihani wa Wizara | 150,000/- | |
| Malipo ya Uhakiki ubora (NACTVET) | 20,000/- | |
| Malipo ya Bima ya Afya | 51,000/ | |
| **Jumla Ndogo** | **221,000/-** | |

- **Hosteli inapatikana ndani ya chuo kwa Tshs 280,000/= kwa mwaka.**
- **Mchango wa bima ya NHIF utalipwa kwa wanafunzi wasiokuwa na bima ya NHIF.**
- **Ada ya hosteli haijumuishi chakula, Chakula kitapataikana chuoni kwa gharama nafuu.**

**RATIBA YA MALIPO – KOZI YA MAABARA TIBA KWA MWAKA 2026/2027.**

Ada zetu zinalipwa kwa awamu nne hadi kumi na tunapokea malipo ya kila mwezi.

Awamu za malipo zimegawanywa kwa vipindi vya miezi mitatu mitatu.

Kama utakuwa na mahitaji ya kulipa kwa zaidi ya awamu nne, Unapaswa kuwasiliana ofisi ya muhasibu.

**Tafadhali zingatia ratiba ya malipo kama ilivyoelekezwa. Ada zote zilipwe katika akaunti husika.**

| **MAELEZO** | **AWAMU YA 1** | **AWAMU YA 2** | **AWAMU YA 3** | **AWAMU YA 4** | **AKAUNTI NAMBA ZA MALIPO** |
|---|---|---|---|---|---|
| | **Okt. – Dis.** | **Jan. – Mach.** | **Apri. – Jun.** | **Jul. – Agost.** | |
| ADA | 550,000/= | 400,000/= | 350,000/= | 100,000/= | **Namba ya Akaunti:** 0150388644200 – CRDB<br>**Jina la Akaunti**: Amenye Health Training Institute |
| MICHANGO MINGINE | 565,000/- | 400,000/- | | | **Jina la Akaunti:** Amenye Health Laboratory<br>**Namba ya Akaunti** : 0150422045300 – CRDB |
| BIMA YA AFYA (NHIF) | 51,000/- | | | | |
| MTIHANI WA WIZARA NA UHAKIKI UBORA | 20,000/- | | 150,000/- | | |
| **JUMLA** | **1,186 ,000/=** | **800,000/=** | **500,000/=** | **100,000/=** | |

**HOSTELI.**

| **MUHULA WA MASOMO** | **KIASI** | **AKAUNTI YA KULIPIA** |
|---|---|---|
| Muhula wa 1 | 140000/- | **Jina la Akaunti:**<br>Amenye Health Laboratory<br>**Namba ya Akaunti :**<br>0150422045300 – CRDB |
| Muhula wa 2 | 140000/- | |

**FEDHA YA TAHADHALI.**

Kila mwanafunzi anatakiwa kulipa fedha ya tahadhari (caution money) ambayo HAIRUDISHWI. Endapo hasara au uharibifu utazidi kiwango hicho, mwanafunzi atalazimika kulipa ziada. Hulipwa wakati wa usajili

**NIDHAMU.**

Taasisi haitasita kuchukua hatua za kinidhamu dhidi ya mwanafunzi yeyote atakayekiuka kanuni na taratibu/sheria za taasisi. Kila Mwanafunzi atalazimika kusaini kanuni za chuo kabla ya kuanza masomo. Kutokujua sheria hakutakubalika kama kisingizio.

**SARE ZA MWANAFUNZI.**

Sare zitazingatia mwongozo wa Wizara ya Afya kwa wanafunzi wa afya (NTA Level 4 - 6).

**Mwanamke:**

Gauni la tetron nzito nyeupe, lenye mikono mifupi.

Hakikisha gauni linavuka magoti – inch 2 chini ya goti, lisiwe na mpasuo nyuma.

Mshono wake uwe sawa na sare za wauguzi .Viatu vyeusi vyenye visigino vifupi, soksi nyeupe na ndefu.

Koti (Lab. Coat) Jeupe lililoshonwa kwa tetron nzito nyeupe. Koti liwe refu na mikono mirefu.

**Mwanaume:**

Suruali yenye rangi ya khaki Tetron upana chini iwe inchi 7 ama 14 cm na kuendelea.

Mwanafunzi hatakiwi kushona suruali inayo bana (Modo). Shati jeupe lenye mikono mifupi.

Viatu vya ngozi vyeusi na soksi nyeusi.

Koti (Lab. Coat) Jeupe lililoshonwa kwa tetron nzito nyeupe. Koti liwe refu na mikono mirefu.

‘Jeans’ siyo vazi la kuvaa darasani au wakati wa mazoezi kwa vitendo hospitalini.

**UCHUNGUZI WA AFYA.**

Mwanafunzi anatakiwa kufanyiwa uchunguzi wa afya katika hospitali ya serikali au binafsi. Fomu iliyojazwa kikamilifu iwasilishwe wakati wa usajili (Fomu imeambatanisha pamoja na fomu hii).

**SERIKALI YA WANAFUNZI (AMSO).**

Serikali ya wanafunzi (Amenye Student Organization – AMSO) inashughulika na masuala yote yanayohusiana na uongozi wa wanafunzi pamoja na vikundi mbalimbali vya wanafunzi. Aidha, serikali ya wanafunzi hutekeleza jukumu la kuunganisha na kuimarisha mawasiliano kati ya wanafunzi na uongozi wa taasisi, Na kuhakikisha utekelezaji na usimamizi wa katiba na kanuni ndogo (by-laws) za wanafunzi kwa mujibu wa taratibu zilizowekwa.

# TAASISI YA MAFUNZO YA AFYA AMENYE - MBEYA

**Namba za Simu** +255742164518 / +255766963739 **Barua Pepe:** amenyetraining@gmail.com
**Anuani**: S.L.P 26 Mbeya, **Eneo:** Mbeya Mjini, Airport ya Zamani **Tovuti:** www.amenyeinstitute.ac.tz

## MEDICAL EXAMINATION FORM FOR THE ACADEMIC YEAR 2026/2027.

To be completed by a doctor and should be submitted to the Admission office during registration.

FULL NAME OF STUDENT ……………………………………………………………………

SEX: MALE/FEMALE ……………………………………………..

HB TEST ………………………………………………………………

STOOL ………………………………………………………………

URINE MICRO …………………………………………………..

H.B.TEST ………………………………………………………………

EYE EXAMINATIONS……………………………………………..

E.N.T …………………………………………………………………..

CHEST X-RAY ………………………………………………….

ABDOMEN ………………………………………………………….

**ADDITIONAL INFORMATION:**

Physical Defects or Impairments, Infections, Chronic, or Hereditary (family) Disease.

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

I certify that I have examined the above Student and consider that he/she is physically/not physically fit for further studies.

DATE ………………………………………….……….. SIGNATURE…………………………………………

STATION…………………………………………….

**Designation**…......................................................................... **And Stamp** …………..

# TAASISI YA MAFUNZO YA AFYA AMENYE - MBEYA

**Namba za Simu** +255742164518 / +255766963739 **Barua Pepe:** amenyetraining@gmail.com
**Anuani**: S.L.P 26 Mbeya, **Eneo:** Mbeya Mjini, Airport ya Zamani **Tovuti:** www.amenyeinstitute.ac.tz


## FOMU YA TAMKO LA MZAZI/MLEZI/MFADHILI.

Mzazi/Mlezi/Mfadhili anatakiwa kuthibitisha kukubali mwanafunzi kufuata kanuni na taratibu zote za chuo. Ukiukwaji wowote unaweza kusababisha mwanafunzi kufukuzwa chuoni.

### TAARIFA ZA MWANAFUNZI.

| Taarifa | Jaza | Taarifa | Jaza |
|---|---|---|---|
| Jina la Familia (Surname) | ______________________ | Majina Mengine (Other Names) | ______________________ |
| Hali ya Ndoa | ______________________ | Jinsia | ______________________ |
| Tarehe ya Kuzaliwa | ______________________ | Ulemavu (ikiwa upo) | ______________________ |
| Mahali pa Kuzaliwa | ______________________ | Uraia | ______________________ |

### TAARIFA ZA MZAZI/MLEZI/MFADHILI.

| Taarifa | Jaza | Taarifa | Jaza |
|---|---|---|---|
| Jina la Familia: | ______________________ | Majina Mengine: | ______________________ |
| Hali ya Ndoa: | ______________________ | Jinsia: | ______________________ |
| Mahali pa Kuzaliwa: | ______________________ | Uraia: | ______________________ |
| S.L.P (Sanduku la Posta): | ______________________ | Namba ya Simu ya Mkononi: | ______________________ |
| Mtaa: | ______________________ | | |
| Kata: | ______________________ | Wilaya: | ______________________ |
| Mkoa: | ______________________ | | |

### TAMKO LA MZAZI / MLEZI / MFADHILI.

Mimi, **(Jina kamili)** ……………………………………………………………………

Mzazi / Mlezi / Mdhamini wa **(Jina la Mwanafunzi)** ………………………………………………………………

Nathibitisha kwa dhati kuwa **nakubali mwanafunzi tajwa hapo juu kujiunga na Chuo**, na ninaelewa kuwa anapaswa **kufuata, kuzingatia na kutii kanuni, taratibu na sheria ndogo (by-laws) za chuo** kama zilivyoainishwa.

Aidha, ninafahamu kuwa **ukiukwaji wowote wa kanuni, taratibu au sheria ndogo za chuo** utasababisha **kufukuzwa kwa mwanafunzi kutoka chuoni** bila madai yoyote.

**Sahihi ya Mzazi / Mlezi / Mdhamini**: ………………………………**Tarehe**: ………………………………